



EAST AFRICAN COMMUNITY

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**WAANGALIZI WA UCHAGUZI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI
KATIKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA UTAKAOFANYIKA TAREHE
28 OKTOBA, 2020**

26 OKTOBA, 2020

Ndugu wana Habari, habari za asubuhi,

- Naomba kuanza kwa kuwashukuru kwa kuitikia wito wetu na kuhudhuria kikao hiki cha waandishi wa habari.
- Napenda pia kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya ya kuelimisha umma wa wananchi wa Afrika Mashariki juu ya umuhimu na faida za mtangamano wa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.
- Ibara tatu (3), aya ya 3 (b) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka Nchi Wanachama wa Jumuiya kuheshimu kanuni za utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na vile vile haki ya kijamii. Pia, Ibara ya sita (6) ya mkataba huo inasisitiza nchi wanachama kufuata kanuni za utawala bora, pamoja na kuheshimu demokrasia, sheria, uwajibikaji, uwazi, haki ya kijamii, usawa wa fursa, usawa wa kijinsia pamoja na kutambuliwa, kukuza na kulinda haki za binadamu kulingana na Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (the African Charter on Human and Peoples' Rights).
- Katika utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiyaya Afrika mashariki Nchi Wanachama zimekubaliana juu ya vigezo vya Uchaguzi huru na wa haki. Hivyo, kila nchi mwanachama inapokuwa na zoezi la uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge, Jumuiya ya Afrika Mashariki hutuma watazamaji wa uchaguzi ili kuhakiki kama

umezingatia vigezo vilivyokubaliwa, sheria na Katiba ya Nchi husika. Huu ndio msingi wa uwepo wa timu ya watazamaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika uchaguzi huu.

- Zoezi hili halilengi tu kukosoa bali pia ni sehemu ya kujifunza ili yale mazuri yatakayobainika Jumuiya izishauri nnchi nyingine kuiga na pale kutakapobainika mapungufu Nchi Mwanachama husika ashauriwe kuchukua hatua za kurekebisha ili zisijirudie tena.
- Ndugu wanahabari, Timu ya watazamaji kutoka Jumuiyaya Afrika Mashariki ina Waangalizi 59, wanaotoka katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Mabalozi wa Vijana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, viongozi wa vijana, wawakilishi kutoka Wizara zinazohusika na Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Nchi wanachama, Tume za Kitaifa za Uchaguzi, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Waangalizi hawa wamegawanywa katika mikoa ifuatayo: Dar es Salaam, Tanga, Unguja, Pemba, Lindi / Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kigoma, Singida, Kilimanjaro, Morogoro na Mwanza.
- Kama nilivyoeleza awali Dhumuni la Waangalizi hawa ni kufanya uangalizi wa mchakato mzima wa uchaguzi, kutoa tathmini iliyo sawa na kamili, kubaini changamoto, udhaifu na fursa ambazo zinaweza kujumuishwa kama mafunzo bora katika mchakato wa uchaguzi na Bodi za Usimamizi wa Uchaguzi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Jumuiya ya Afrika Mashariki pia ina dhumuni la:
 - (a) Kujenga imani ya wananchi katika michakato mzima wa uchaguzi kwa kuhamasisha wapiga kura na wadau wengine kushiriki kwa uhuru katika uchaguzi, na katika mazingira ambayo yanakuza ushindani na uvumilivu bila vitisho au uvunjifu wa amani;
 - (c) Kutoa mapendekezo ya kuimarisha mchakato mzima wa uchaguzi kwa sio tu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Kuanzia Oktoba 24 hadi 25, Waangalizi wa Uchaguzi wa EAC wamepokea mafunzo kabla ya kuanza rasmi zoezi la uangalizi tarehe 26 Oktoba, 2020.
- Timu ya Watazamaji wa Uchaguzi wa EAC inaongozwa na **Mh. Sylvestre NTIBANTUNGANYA**, Rais Mstaafu wa Jamuhuri ya Burundi.

- Naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba watanzania wote na hasa vijana, kuzingatia na kuipa kipaumbele amani katika kipindi hiki.

Asanteni Sana